# Mahusiano ya Vijana wa Jinsia Tofauti katika Nathari za Kiswahili

*Justus Kyalo Muusyaa*
*Chuo Kikuu cha Kirinyaga*

**Ikisiri**

**Vijana ni wanajamii walio na umri kati ya watoto na watu wazima. Tabaka hili la wanajamii hukabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto hizi hutokana na jaribio lao la kujitambulisha na kujiandaa kwa majukumu ya utuuzima. Changamoto hizi ni pamoja na namna ambavyo vijana wa kike hupaswa kuhusiana na wenzao wa kiume. Vijana wengi hukuza mahusiano haya, mengi yakiwa ya kimapenzi bila ya kujua namna ya kuyaendesha. Matokeo ya mahusiano haya aghalabu huwa ni kuvuruga maisha yao. Suala hili limesawiriwa na waandishi wa nathari za Kiswahili; riwaya sawa na hadithi fupi. Nathari hizi zimeitikiana na kulingana kwa kiwango kikubwa katika usawiri wa jambo hili. Ulingano huu ndio umechunguzwa katika makala haya kwa kuongozwa na nadharia ya usemezano. Makala yamebainisha kuwa kuna usemezako kati ya riwaya na hadithi fupi katika kuonyesha mahusiano ya vijana wa jinsia tofauti. Riwaya moja na hadithi mbili zimetumiwa katika makala. Riwaya ni ile ya *Taswira za Mawingu* (2011). Hadithi nazo ni 'Kanda la Usufi' kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007) na 'Mapenzi ya Kifaurongo' katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Makala yamechunguza ni kwa kiwango gani nathari hizi zimeshughulikia mahusiano ya vijana kwa namna inayolingana.**

**Maneno Muhimu:** Nathari, Mahusiano, Vijana, Jinsia, Usemezano.

**Utangulizi**

Makala haya yamechunguza mahusiano ya vijana katika nathari za Kiswahili. Nathari ni kazi za kubuni ambazo hutumia lugha ya kimaelezo, kimfululizo na kiinsha tofauti na iliyo katika ushairi (Balisidya, 1983). Ni lugha iliyo tofauti na ya ushairi; lugha ya moja kwa moja na ya kawaida. Lugha ya nathari hutumiwa katika uandishi wa tungo kama vile riwaya na hadithi fupi. Tungo za aina hii ndizo zimehakikiwa katika makala haya. Zilizotumiwa kufanikisha uchunguzi huu ni riwaya ya *Taswira ya Mawingu* ya Sinjiri Mukuba (2011) na hadithi fupi mbili. Hizi ni Kanda la Usufi' kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007) na 'Mapenzi ya Kifaurongo' katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Nathari hizi zimeteuliwa kimakusudi kuhakikiwa katika makala haya kwa vile usomaji awali ulibainisha kuwa zilikuwa na data ya kutosha inayotakiwa katika uchunguzi huu. Zimesawiri mahusiano ya vijana kwa kiwango kikubwa huku zikiingiliana na kusemezana sana kwa namna ambavyo zimeshughulikia suala hili.

**Dhana ya Usemezano**

Dhana ya usemezano inayotokana na kitenzi 'semezana'. Kama nadharia ya kuhakiki usemezano ulihasisiwa na mwanaisimu na mhakiki wa fasihi Mikhail Mikhaillovich Bakhtin. Bakhtin aliishi kati ya 1895-1975 ambapo alijitosa katika uandishi baada ya mapinduzi ya Urusi ya 1917.

Katika vitabu vyake (1978, 1981, 1984, 1990) Bakhtin alidhihirisha kuwa kazi ya fasihi huwa inatilia mkazo muktadha maalum wa kihistoria na kijamii kwa vile umbo la fasihi huwa ni chombo katika uhakiki wa jamii. Kwa maoni ya Bakhtin (1990), matini zote huwa ni za kiusemezano. Anaeleza kuwa dhana ya usemezano hurejelea mazungumzo kati ya mtu na mwingine katika maongezi ya kila siku. Ni muhimu kutambua kuwa, mazungumzo hufanikiwa kwa kuwepo kwa lugha. Bakhtin alisisitiza kuwa kila wakati lugha huwa na sifa za kiusemezano. Kwa mujibu wake, kanuni ya usemezano huchochea na kutawala katika mazungumzo yoyote yale. Kwa hivyo huwa ni kanuni muhimu sana.

Bakhtin anasisitiza kuwa maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kiusemezano. Kwa mujibu wa mawazo haya, hata tamko la kiuzungumzi nafsia huingiliana kimaana linakopatikana katika mazungumzo. Katika kiwango cha matini, neno fulani linaweza kuwa na maana tofauti katika hatua mbalimbali, katika historia ya lugha au katika hali tofauti za wakati huo huo wa kihistoria.

Nadharia ya usemezano vilevile huzingatia kiwango cha uhusiano uliopo kati ya mazungumzo ya mtunzi, wahusika wake na hadhira yake kwa upande mmoja na kati ya wasomaji wa matini inayohusika na mtunzi wa kazi hiyo kwa upande mwingine.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981 na 1984), kazi ya fasihi ni uwanja ambao una mwingiliano wa matini. Kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyinginezo zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Mwingiliano huu unashirikisha pia mazungumzo ya kila siku yanayotokea kando ya matini zilizorasimishwa. Bakhtin anadai kuwa matini ni uwanja ambao una mwingiliano wa kiusemezano baina ya sauti mbalimbali za matini. Yaani, hakuna matini ambayo ni asilia zaidi. Kila matini inarejelea matini nyinginezo zilizopo, za wakati uliopita na za wakati ujao.

Akichangia nadharia ya usemezano, Michael Holoquist (1990), anakiri mawazo ya Bakhtin kwamba matini huwa ni za kisemezano. Hii ina maana kuwa kila semi ni jibu la kitu kingine na hutarajiwa kujibiwa. Anasisitiza kuwa kila usemezano huwa na sifa ya kutokamilika. Hii ni kwa sababu hakuna kauli ya mwisho, kwani matini zote za kisemezano huwa na uwili wa mwelekeo na mkabala.

Bakhtin anasema kwamba majibizano baina ya msemeza na msemezwa yanatokana na kule kuathiriana kwao (Morson, 1986: 92). Hakuna mtu yeyote anayetoa tamshi halafu akajigamba nalo kwamba yeye ndiye wa kwanza kulisema. Isipokuwa Adamu peke yake ndiye aliyekuwa wa kwanza kutumia maneno kwani yeye ndiye wa kwanza kufunzwa maneno (Bakhtin 1981:279). Mukarovsky (1977) anasisitiza kwamba mahusiano ya msemeza na msemezwa huwa na washiriki angaa wawili ambao hutambuana kama 'mimi' na 'yeye'. Akiunga mkono maneno haya, Pierce (1994) analinganisha usemezano na simu ambapo kuna wahusika wawili, msemaji na msemezwa hupaswa kuwapo ili mazungumzo yaendelee. Mihimili kadha muhimu ya nadharia hii imetumika katika makala haya.

**Taasisi za Elimu**

Kwa mujibu wa nadharia ya usemezano, usemezano huweza kubainika katika matumizi ya sajili mbalimbali katika matini. Waandishi wa nathari zilizoteuliwa kwa uchunguzi huu wamesawiri sajili ya elimu. Mahusiano ya vijana yanajitokeza katika mandhari haya ya shuleni. Mathalan, katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu* tunaelezwa kuhusu mahusiano ya vijana katika shule ya upili. Kwamba Gladys akikuwa mwanafunzi wa shule ya upili, aliweza kujihusisha kimapenzi na mwanaume kwa jina Kanja. Uhusiano wao ulizidi kiasi kwamba akiwa kidato cha tatu aliweza kuambulia ujauzito. Tunaelezwa hivi:

> 'Bwana yule (Kanja) alimringa Gladys miaka miwili iliyopita akiwa kwenye shule ya sekondari kidato cha tatu na kumfanya asitishe masomo yake (Mukuba 2011:62).

Kwingineko katika riwaya hii kuna usawiri wa mahusiano ya vijana katika chuo kikuu. Wake kwa waume waliweza kujihusisha na mapenzi wakiwa chuoni. Hii ndio maana mwandishi anaeleza namna hii:

> 'Baadhi ya wanafunzi wa kiume wa miaka ya nne na tatu walizurura kwenye mabweni ya wanafunzi wa kike kutwa nzima na hata usiku wakibisha mlango… Monii naye alijitosa. Baada ya muda wa miezi miwili hivi alikuwa na mtu wake. Aliitwa Bramwel' (Mukuba 2011:156-157).

Kwenye hadithi ya 'Kanda la Usufi' uhusiano wa wanafunzi katika mandhari ya shule ya upili vilevile yamesawiriwa. Siku ya tamasha za muziki katika shule ya Askofu Timotheo ndipo Chris

Masazu aliweza kufahamiana na Sela. Uhusiano wao uliendelea na kuwa wa kimapenzi. Imesawiriwa kuwa:

> 'Uhusiano wao ulijengeka hapo kivulini. Waliachana baada ya 'maumivu ya kichwa' kumpungua Chris, kila mmoja akiwa na kijikaratasi chenye jina na anwani ya mwenzake' (Nyaga 2007:61).

Hadithi ya 'Mapenzi ya Kifaurongo' vilevile ina usimulizi wa aina hii. Penina na Dennis wanaishia kuwa wapenzi wakiwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kivukoni. Penina ndiye anayemtaka mapenzi Dennis. Anaenda hadi katika chumba alimokuwa akiishi Dennis na kumwambia,

> 'Basi nimekuja kukuambia kuwa moyo wangu umedondokea kwako. Nataka uwe rafiki yangu; rafiki wa chanda na pete, mpenzi wangu wa dhati wa kunifaa na mimi kumfaa kwa jua na kwa mvua' (Wasike 2016:20).

**Mazingira ya Nyumbani**

Mukuba amesawiri namna ambavyo mahusiano ya vijana huweza kupokelewa nyumbani kwao. Hii ni sajili ya nyumbani. Ni sajili majawapo ambapo matini huweza kusemezana katika matini. Aghalabu uhusiano wa kimapenzi miongoni mwa wanafunzi haukukubalika na wazazi nyumbani kwa vile wazazi huweza kutabiri athari zake mbaya. Wazazi hawakuruhusu uhusiano wa Gladys na Kanja kuendelea katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu*. Tunaelezwa,

> '… yeye (Kanja) na Gladys wakaamua kuanza kuishi pamoja, licha ya kwamba wazazi wake Gladys hawakuridhia wala kujadili mpango wowote wa ndoa baina ya hawa wawili' (Mukuba 2011:62).

Katika riwaya hii pia, wazazi wa Monii wanakataa uhusiano wake na Bramwel, wote wakiwa wanafunzi wa chuo kikuu. Hili linatokea Monii alipompeleka mpenzi wake nyumbani kwao akamfahamishe kwa wazazi wake. Mamake Monii anasingizia kuwa wawili hao walitoka katika makabila tofauti na hivyo uhusiano wao haungestahili. Anamuuliza Bramwel:

> "Nyinyi ni watu wa kabila gani?"
>
> "Sisi ni Wasulii."
>
> "Mhm! Sisi ni Wasaki sasa mkiamua kuoana itakuwaje? Mnatoka kwenye tamaduni tofauti. Inawezekana kweli?" (Mukuba 2011: 161).

Nyaga alisawiri suala kama hili katika 'Kanda la Usufi'. Sela anapotiwa mimba na Chris Masazu anafukuzwa shuleni. Kule nyumbani babake alichukulia suala hili kama usaliti mkubwa. Anakana tukio hilo. Ananuia kumfukuza Sela nyumbani akiwa na mamake. Hivi ndivyo ilivyokuwa:

> 'Leo ndio mtanitambua… Mtwae kilicho chenu mniondokee!'

Baadaye wanakijiji waliingilia kati na kumtuliza babake Sela, Mzee Butali. Akakubali kubadilisha nia yake. Halafu:

> 'Sela alikaa nyumbani kwa muda wa miezi mitatu akikitunza kitoto chake' (Nyaga 2007:63).

Wazazi wa Penina vilevile katika 'Mapenzi ya Kifaurongo' wanakataa uhusiano kati yake na mpenzi wake Dennis. Sababu waliyotoa ya kukataa uhusiano huo ilikuwa kwamba wawili hao walikuwa wa matabaka tofauti, Dennis akiwa maskini aliyetazamia kukithiwa mahitaji yake na mpenziwe Penina aliyetoka katika familia ya kitajiri. Penina anakuja kumweleza Dennis hili baadaye. Anamwambia:

> 'Nimewakosea mama na babangu mno. Walikuwa wamenionya dhidi ya kuchubiwa nawe. Nikawapuuza. Sasa nimekuja kujua walichomaanisha' (Wasike 2016:26).

**Usemezano wa Mawazo**

Waasisi wa usemezano wanaamini kuwa waandishi wa kazi za fasihi huandika mambo yaliyozungumziwa na waandishi wengine katika kazi zao. Kwa sababu hii, hakuna kauli ya kifasihi ambayo huwa ya mwisho. Wazo hili linajitokeza katika matini zilizohakikiwa katika makala haya. Mwandishi wa riwaya ya *Taswira ya Mawingu* anasawiri mapenzi baina ya wanafunzi. Anasawiri

kuwa mapenzi haya huweza kuvuruga masomo na maisha yao. Gladys aliweza kutiwa mimba na Kanja. Kanja alikuwa tayari amekamilisha masomo yake ya shule ya upili. Lakini Gladys alikuwa kidato cha tatu. Gladys alilazimika kukatiza masomo yake kwa muda ili akailee mimba na kumlea mtoto alipozaliwa ndipo kurudi shuleni kuendelea na masomo yake. Tunaelezwa:

> 'Gladys alipokwisha kujifungua… akarudi shuleni kumalizia elimu yake ya shule ya upili. Ilivyokuwa kwamba mahaba yake na bwana huyu ambaye ashamaliza elimu ya shule ya upili mbele yake yalikuwa yakiendelea …' (Mukuba 2011:62).

Namna ambavyo mapenzi huvuruga masomo imesawiriwa na Nyaga kwenye hadithi ya 'Kanda la Usufi'. Sela alilazimika kutafutiwa shule ya kutwa baada ya kufukuzwa katika shule yake ya awali alipopata himila. Mwandishi anasema:

> 'Shule ilipopatikana, Sela alihudhuria masomo hadi pale ilishindikana; siku za kujifungua zilipokaribia…' (Nyaga 2007:63).

Wazo la kulelewa kwa mtoto wa Gladys katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu* na kulelewa kwa mtoto wa Sela katika hadithi ya 'Kanda la Usufi' linasemezana. Mtoto wa Gladys, Monique alilelewa kwa muda na halatiye Keti huko nyumbani kwa wazazi wake. Huu ni wakati ambapo Gladys alirudi shuleni kumalizia masomo yake ya shule ya upili, na baada ya masomo hayo akaenda kuishi na mpenziwe Kanja mjini (uk.62). Vivyo hivyo, Kadogo, mtoto wa Sela katika hadithi ya 'Kanda la Usufi' alilelewa na halatiye Rozina kuko huko nyumbani kwa wazazi wa Sela. Alirejea shuleni akamaliza masomo ya shule ya upili kama alivyofanya Gladys na kwenda kuishi na mpenzi wake Chris Masazu mjini (uk. 64).

Vilevile, mhusika Kanja katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu* alipomaliza masomo yake ya shule ya upili alihamia katika mji wa Deja kutafuta kibarua. Hivi ndivyo tunavyoelezwa:

> 'Bwana yule ambaye kwao kulikuwa kijiji jirani, baada ya kukamilisha elimu yake ya upili mwaka mmoja uliopita alihamia mjini Deja, zapata kilomita mia mbili hamsini kutoka kijijini pale, kwenda kutafuta kibarua. Alipata kibarua cha kuvuna mkonge ambacho mshahara wake haukuwa chochote kando na kumwezesha kulipa kodi ya chumba kimoja kidogo na kununua chakula,' (Mukuba 2011: 63).

Chris Masazu alifanya kama alivyofanya Kanja. Alihamia mjini Dafina kutafuta kibarua kama ambavyo mwandishi anasema:

> 'Masazu alitoka katika kijiji jirani na cha kina Sela. Baada ya kukamilisha elimu yake ya shule ya upili, alihamia mjini Dafina kuenda kutafuta kibarua. Alipata kibarua cha kuvuna mkonge ambacho mshahara wake haukuwa chochote kando na kumwezesha kulipa kodi ya chumba kimoja kidogo na kununua chakula' (Nyaga 2007:63).

Nukuu hizi zinapiga mwangwi usawiri kuhusu Gladys na Kanja katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu*. Tunaelezwa kuwa, kutoka mjini Deja, Gladys na Kanja waliamua kuja nyumbani kwa akina Gladys kumchukua mtoto wao kutoka kwa halatiye Keti wakati wa usiku kama inavyoonyeshwa katika riwaya ya *Taswira za Mawingu*. Walikuja mwendo wa saa tano usiku. Tendo kama hili linafanywa na Sela na Masazu. Wanatoka mjini Dafina kuja kumchukua mtoto wao Kadogo kutoka kwa halatiye Rozina wakati wa usiku katika hadithi ya 'Kanda la Usufi'. Walisubiri hadi mwendo wa saa sita za usiku. Inaelekea kuwa jozi hizi mbili za wazazi zilitumia njia ya mkato kuwapata watoto wao ili kukwepa kufuata utaratibu unaokubalika na jamii wa kuchukua watoto wao. Hizi hapa nukuu:

> 'Walipofika dirishani, bwana yule alibisha taratibu huku akimwita halatiye Monique kwa mnong'ono, "Keti, Keti, Ketii!" (Mukuba: 2011).

Upande mwingine katika hadithi fupi tunaambiwa,

> 'Walipofika dirishani, Masazu alibisha taratibu huku akimwita halatiye Kadogo kwa mnong'ono, "Rozina, Rozina, Rozina!"' (Nyaga 2007:64).

Keti, kama alivyo Rozina alikuwa amelala walipokuwa wakiamshwa na wazazi wa watoto waliokuwa wakiwalea. Baada ya muda wote waliweza kuamka. Kila mmjoa wao alitaka kuhakikisha kuwa mama mtoto alikuwa. Hii ni kwa sababu akina baba wa mtoto ndio waliokuwa wanaita dirishani. Katika *Taswira ya Mawingu* inaelezwa namna hii:

> 'Keti aligutuka akanyanyuka kitandani taratibu, naye pia akaitikia kwa mnong'ono, "Naam, naam shemeji Kanja." Kwa mnong'ono ule ule akauliza, "Umekuja na dada Gladys?"
>
> "Ndiyo. Ninaye," jawabu likaja. Keti akafungua dirisha mwanya na kuthibitisha uwepo wa dada yake. Wakapungiana mikono kwa salamu, japo hawakuonana barabara mle gizani (Mukuba 2011: 65).

Upande mwingine, wazo hili linasawiriwa kwa lugha sawa na iliyotumiwa katika riwaya, kwenye hadithi ya 'Kanda la Usufi' namna nii:

> 'Rozina aligutuka na kunyanyuka kitandani taratibu, naye pia akaitikia kwa mnong'ono, "Naam, naam shemeji Masazu." Kisha, kwa mnong'no ule ule akauliza, "Umekuja na dada Sela?"
>
> "Ndiyo. Ninaye," jawabu likaja. Rozina akafungua dirisha na kuthibitisha uwepo wa dada yake, na wakapungiana mikono kwa salamu, japo hawakuonana barabara mle gizani (Nyaga 2007: 64).

Nukuu hizi zinaonyesha usemezano wa kiwango cha juu, usemezano unaopiku ule wa kisadfa kwa namna ambavyo unatokea kuwa wa moja kwa moja kwa vile lugha inayotumiwa inafanana kabisa. Kwa namna sawa, waandishi hawa wanaeleza kwamba watoto waliokuwa wamekuja kutwaliwa na wazazi wao, Monii na Kadogo walikuwa wamelala wakati huo. Walezi wao waliwachukua polepole na kwapitishia dirishani na kuwakabidhi kwa akina baba zao. Kisha walezi wakarudi kulala.

**Usemezano wa Mandhari ya Hali na Wakati**

Kwa mujibu wa nadharia ya usemezano, kila matini aghalabu huwa ni jibu la matini tangulizi na ambalo hutarajiwa kujibiwa na matini zingine za baadaye. Kujibizana huku kwa matini tangulizi na matini za baadaye kunajitokeza katika usawiri wa mandhari ya hali na wakati kwenye nathari zinazohakikiwa katika makala haya. Mukuba na Nyaga wanasawiri majira ya mvua kubwa katika mandhari ya usiku. Haya ni ya wakati wazazi walipoamua kwenda kuwachukua watoto wao kutoka kwa akina nyanya zao. Hali hii ilikuwa kizingiti katika juhudi zao, na hivyo kuzua changamoto usiku. Walinyeshewa sana kando na barabara kuwa na utelezi. Maji yaliyotuama barabarani yalikuwa tatizo lingine. Hii ilikuwa ni adhabu kwa wazazi hawa kwa kutofuata mila na desturi za jamii zao. Katika riwaya imeelezwa:

> 'Walifika sehemu ambapo mti ulikuwa umeanguka na matawi na majani yake kukingama njiani. Walisita. Baba yake Monique aliyapigapia yale majani kwa bakora aliyokuwa nayo ili kujaribu kubainisha wangelikopenyea. Alitoa kiberiti chake cha petroli cha sigara mfukoni akawasha mpigo mmoja ili kupata mwanga. Akaruka yeye kwanza na kwenda upande wa pili wa mti… akaelekea upande wa kulia lakini ghafula akagundu palikuwa na dimbwi la maji yaliyotuama pale' (Mukuba 2011: 66-67).

Maelezo kama haya yanajitokeza katika hadithi ya 'Kanda la Usufi' kwa njia inayolandana na nukuu iliyo hapo juu kutoka kwa *Taswira ya Mawingu*:

> 'Walifika sehemu ambapo mti ulikuwa umeanguka na matawi na majani yake kukingama njiani. Walisita. Masazu aliyapigapia yale majani kwa bakora aliyokuwa nayo ili kujaribu kubainisha wangelikopenyea. Alitoa kiberiti chake cha gesi cha kuwashia sigara mfukoni akawasha mpigo mmoja ili kupata mwanga. Akaruka yeye kwanza na kuenda upande wa pili wa mti … akaelekea upande wa kulia lakini ghafla akagundua palikuwa na dimbwi la maji yaliyotuama pale' (Nyaga 2007: 66).

**Usemezano katika Usawiri wa Maumbile**

Baadhi ya kazi za fasihi huweza kuingilia na kazi zingine. Hizi zinaweza kuwa ni zile ambazo zilizitangulia kuandikwa ama zile ambazo zilizifuata kuandikwa. Usemezano wa aina hii unajitokeza kati ya riwaya ya *Taswira ya Mawingu* na hadithi ya 'Mapenzi ya Kifaurongo'. Nathari hizi zimeingiliana kwa namna ambavyo zimesawiri taswira kuhusu urembo wa wasichana wa vyuo vikuu ambao wanaishia kuwa na wapenzi miongoni mwa wanafunzi wenzao. Mhusika Monique au Monii, mwanafunzi wa chuo kikuu cha Rishna anasawiriwa namna hii kwenye riwaya.

> 'Kwa sasa Kulesoni alikuwa akimtazama kwa uwazi pasi na kuficha. 'Maziwa si manene, si madogo; ni ya kadiri.' Kulesoni alijisemea' (Mukuba 2011: 196).

Katika hadithi urembo wa msichana unaelezwa hivi:

> 'Lo! Mlangoni yuko msichana mmoja mrembo. Umbile la mwili wake linadhihirisha siha nzuri aliyonayo. Amekatika kike na kulegea kama wanawake niwaonao kwenye runinga na majarida. Ameumbwa akaumbika. Mtazamo wake unaweza kumwamsha mbwa aliyelala' (Wasike 2016:18).

Vijana wa kike wanaanzisha uchumba na wale wa kiume wakiwa chuoni walitekeleza majukumu muhimu katika kuwakimu wapenzi wao kifedha. Hii ni kwa sababu waandishi wamezichora familia zo zikiwa imara kiuchumi kuliko zile walizotoka wapenzi wao wa kiume. Utegemezi huu ulikuwa kigezo mojawapo wa vigezo vilivyopalilia mahusiano yao hata yakadumu kwa muda wote huu. Wasichana walitumia pesa walizopewa na wazazi wao kujikimu kuwakimu wachumba wao. Kwa mfano tunaambiwa hivi:

> 'Hata hivyo, licha ya Monii kukataa kwenda na wazazi wake, walimpatia hela ambazo zingemwauni na kumwambia wapange na Kulesoni kwenda kuwatembelea ili mipango kamili ya kuoana kwao ifanywe…' (Mukuba 2011: 228).

Katika hadithi inasimuliwa hali kama hii.

> 'Mimi na Penina tunaishi mtaa wa New Zealand… Lakini kodi yetu hulipwa na wazazi wa Penina kwa kuwa bado hatujapata kazi' (Wasike 2016:22).

Kazi hizi za fasihi zimeonyesha usemezano katika namna ambavyo mahojiano ya kuwaajiri wafanyikazi huendeshwa katika mashirika mengi. Vijana wa kiume ambao walikuwa na wapenzi wao tangu wakiwa chuo kikuu ndio wanaenda kwa mahojiano katika riwaya na hata katika hadithi fupi. Wote walikuwa wahitaji. Walienda kwa mahojiano baada ya kuhitimu vyema vyuoni. Walikuwa na matumaini ya kupata kazi, jambo ambalo lingewawezesha kudumisha uhusiano wao na wapenzi wao. Hata hivyo walikuwa bado hawakuwa wameoana. Wote waliweza kushindana na vijana wa kike katika mahojiano hayo, kama ilivyoonyeshwa na Mukuba 2011: 223 na Wasike 2016:23, 25. Hata hivyo, wote waliweza kushindwa na wenzao hao wa kike.

Mahusiano kati ya vijana wa kike na wa kiume yanasambaratika baada ya vijana wa kiume kukosa kupata ajira. Inatokea kuwa wachumba wao hawangeendelea kuwakimu mahitaji yao kwa vile walitarajia kwamba waume zao wangepata kazi na kuanza kuendesha mahusino yao kiuchumi. Katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu* Monique anamwacha Kulesoni waliyekuwa wanaishi pamoja wakichumbiana baada ya kumwambia maneno haya kwa njia ya barua:

> 'Mimi nimechoka. Nimechoka kuishi na mtu ambaye hana malengo maishani. Hakika wewe si Kulesoni niliyemjua siku za chuoni. Kwa utepetevu wako sioni hali ikibadilika. Sikutegemea ungeniongoza kuishi maisha ya ufukara kiasi hiki. Fahamu kwamba sikufukuzwa kwetu narudi huko. Chukulia kama hatukujuana. Kwaheri' (Mukuba 2011: 232-233).

Wazo hili limeradidiwa katika hadithi fupi. Tunasimuliwa namna ambavyo Penina alimfukuza Dennis alipokosa kupata kazi baada ya kualikwa mahojiano. Penina katika 'Mapenzi ya Kifaurongo' akimfukuza Dennis anamweleza hivi:

> "Nimechoka kuishi maisha haya… Nilikupenda nikidhani utapata kazi, kumbe ni wewe ni kiumbe asiye na maana yoyote… Kwa sababu hii, sioni haja yoyote ya kuishi nawe. Naomba tafadhali uchukue chochote unachokiona chako, ujiendee zako… Tena tafadhali usije ukamwambia mtu uliwahi kuwa mpenzi wangu." (Wasike 2016: 26-27).

Tofauti hapa ni kwamba katika riwaya kijana wa kike ndiye anajiondoa na kwenda ilhali katika hadithi fupi yule wa kiume anafukuzwa ili ajiondoe.

**Usemezano Kiwango cha Kauli**

Kauli mbalimbali za kazi ya fasihi huweza kuingiliana na za kazi nyingine tangulizi au zinazofuata. Katika *Taswira ya Mawingu* mwandishi anatoa kauli hii,

> 'Bramwel alimhakikishia Monii kwamba daima yu naye' (Mukuba: 2016:165)

Na katika hadithi ya 'Kanda la Usufi' mwandishi anatoa kauli sawa na hii:

> 'Masazu alikichomeka kidole chake cha shahada ardhini, akakilamba kisha akamtazama Sela machoni barabara.' Ndipo Masazu akamwambia Sela, 'Mahaba yangu kwako ni ya dhati' (Nyaga 2007:61).

Katika ofisi ya mahojiano, Kulesoni katika riwaya ya *Taswira ya Mawingu* anaagizwa:

> "Nipe vyeti vyako." Kisha anaulizwa "Kwa nini unadhani kwamba unafaa zaidi kupewa kazi ya ukarani katika kampuni yetu?' (Mukuba 2011:223).

Kauli kama hizi zilielekezwa kwa Dennis alipokwenda kwa mahojiano katika kampuni ya uchapishaji wa magazeti. Aliagizwa:

> 'Leta nyaraka zako.' Kisha akaulizwa: 'Hebu nieleze sababu iliyokufanya utafute kazi katika shirika hili.' (Wasike: 2016: 25).

**Hitimisho**

Uchunguzi huu umebainisha kuwa mahusiano mengi ya vijana wa kiume na wale wa kike yanahusu mambo ya mapenzi. Aghalabu mahusiano haya huweza kuanzia katika taasisi za elimu kama vile shule za upili na vyuo vikuu, kisha huweza kuendelea nje ya taasisi hizi kama vile nyumbani na mijini. Katika mhusiano haya, imeweza kuonyeshwa kuwa vijana wa kike wana jukumu kubwa katika kudumisha mahusiano hayo, hasa mahusiano hayo yakiwa katika hatua za mwanzomwanzo. Vilevile, katika hali zote hizi, mahusiano ya vijana wa kike na wa kiume hupingwa vikali na wazazi wa vijana wa kike. Aidha, mahusiano hayo huweza kuwa na athari mbaya kama vile kutunga mimba isiyotakiwa, na ambayo huishia kuvuruga masomo ya vijana wa kike. Imebainika pia kwamba waajiri wengi wanawapendelea vijana wa kike waliosoma kuliko wenzao wa kiume wenye elimu sawa kutokana na sababu mbalimbali.

Mahusiano ya vijana yanaathiriwa na ukabila. Baadhi ya wazazi wana hisia za kikabila. Wanashikilia kuwa watoto wao wanapaswa kuhusiana na wenzao kutoka kabila lao. Hivyo, wanapinga hali ambapo watoto wao watajiingiza katika mahusiano ya aina yoyote, yakiwemomahusiano ya kimapenzi na ndoa na vijana wenzao wasio wa kabila lao. Vilevile mahusiano ya vijana yanaathiriwa na utabaka. Wazazi wanaona kuwa watoto wao hawapaswi kujiingiza katika mahusiano na vijana walitoka katika tabaka la chini kiuchumi kuliko lao. Badala yake wazingatie tabaka saw ana lao katika mahusiano yao. Hivyo, ni wazi kuwa wazazi wanajibidiisha kuelekeza mkondo wa mahusiano ya watoto wao japo wanashindwa. Wanashindwa kwa vile vijana nao wangetaka kujiamulia mustakabali wao na kuwa huru na wazazi wao.

Mahusiano mfano wa mapenzi miongoni mwa vijana walio shuleni na katika taasisi nyingine za masomo kama vile vyuo vikuu yanaathiri masomo yao. Masomo yanapovurugika, mahusiano ya vijana hawa na wazazi wao yanavurugika pia. Jambo hili linaathiri mshikamnao wa familia zao.

**Marejeleo**


Bakhtin, M.M. (mh) (1981). *The Dialogic Imagination: Michael Holoquist.* Austin: University of Texas Press.

Bakhtin, M.M. (1984 Ed) *Problems of Dostoevsky's Poetics. Theory and History of Literature Vol.* Minneapolis: University of Minnesota Press.

Bakhtin, M.M. (mh) (1986) *Speech Genres and other late Essays*. Austin: University of Texas Press

Bakhtin, M.M. (1990). *Art and Answerability*. Austin: University of Texas Press.

Balisidya, M. L., (1983). *Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Chokocho, A. Kayanda D. (2004). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Clark, K. & Michael, H. (1984). *Mikhali Bakhtin*. Cambridge: Harvard University Press.

Holoquist, M (1990). *Dialogism: Bakhtin and His World*. London: Routledge.

Medvedev P.N & Bakhtin M.M (1978). *The Formal Method in Literacy Scholarship: A Critical Introduction to Socialogical Poetics* Bartimore: John Hopkins Press

Morson, C. (1980) (ed). *Bakhtin Essays and Dialogues of His Work*. Chicago: The University of Chicago Press

Morson, G.S. Caryl. (1990). *Mikhail Bakhtin, Creation of Prosaics* Stanford University press

Mukuba, S. (2011). *Taswira za Mawingu*. Nairobi: Moran Publishers.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.

Pearce, L. (1994). *Reading Dialogics*. Toutledge: Chapman and Hall inc.

Walibora, K. Mohamed S. (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Moran Publishers.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers: Nairobi.